# SCHOOL BASED ASSESSMENT

# KISWAHILI
# SEHEMU B

**(For Regular Learners and Learners with Physical Disability)**

# Gredi ya 4 – 2024

**JINA LA MWANAFUNZI :** ________________________**GREDI :** ______________

**NAMBARI YA TATHMINI:**_______________________________________________

**TAREHE:**______________________________________________________________

**JINA LA SHULE:** _______________________________________________________

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

**JEDWALI LA ALAMA**

| | ZOEZI 3: UFAHAMU WA KUSOMA | ZOEZI 4: SARUFI | ZOEZI 5: KUANDIKA |
|---|---|---|---|
| **Swali** | **1-16** | **17-30** | **31** |
| **Upeo** | **16** | **14** | **10** |
| **Alama za mwanafunzi** | | | |
| **Kiwango Cha Utendaji** | | | |


**Tathmini hii ina kurasa 10 zilizopigwa chapa.**

**Geuza ukurasa**


*©2024 The Kenya National Examinations Council*

## ZOEZI 3: UFAHAMU WA KUSOMA

**Swali la 1 hadi la 4**
*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*



Bendera yetu ya Kenya inapendeza. Rangi zake zinavutia hasa inapopepea. Bendera yetu ina rangi nne. Je, **unazifahamu** rangi za bendera yetu? Rangi ya kwanza ni nyeusi, ya pili ni nyeupe, ya tatu ni nyekundu na ya nne ni kijani.

Kila rangi katika bendera yetu ni muhimu. Rangi nyeusi inaonyesha rangi ya ngozi yetu. Rangi nyeupe ni ya amani. Tulipata amani baada ya kupigania uhuru wa nchi yetu. Rangi nyekundu inatukumbusha damu iliyomwagika wakati wa vita vya ukombozi. Rangi ya kijani nayo, inaonyesha ardhi yetu.

Bendera yetu ina ngao na mikuki miwili. Hii ni ishara ya umoja na ulinzi wa uhuru wetu. Ina maana kuwa, sisi Wakenya tuko imara na tayari kuutetea uhuru wetu. Tunajivunia bendera yetu.

1. Bendera ya Kenya ina rangi nne. Je, rangi ya tatu ni gani?

   ______________________________________________________________

2. Je, ni kwa nini tunajivunia bendera yetu?

   ______________________________________________________________

3. Mwenzako anacheza wakati bendera inapandishwa. Je, utafanya nini?

   ______________________________________________________________

 *©2024 The Kenya National Examinations Council*

4. Wakenya tuko imara na tayari kuutetea uhuru wetu. Hii ina maana kuwa Wakenya ni: (mashujaa, wazalendo)

________________________________________________

**Swali la 5 hadi la 8**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*



Hapo zamani Kanga aliishi kwa Binadamu. Kanga alipewa chakula, makao na ulinzi. Kanga alifurahia maisha haya. Kila mara aliwaambia ndege wa porini kuhusu wema wa binadamu. Hata rafiki yake, Tausi, alitamani kuishi na binadamu.

Wakati mmoja, mvua ilikosa kunyesha kwa muda. Kiangazi kilizidi na ardhi ikakauka. Binadamu na Kanga walikosa maji na chakula. Njaa ilizidi. Walishauriana kuhusu namna ya kutafuta chakula.

"Ndugu, Tausi ameniambia kuwa huko porini kuna chakula kingi. Naona ni heri niende huko. Huenda nikapata chochote. **Kitatufaa.**" Kanga alisema.

"Nenda ndugu yangu. Mwenyezi Mungu atujalie." Binadamu alisema.

Kanga alichukua mkoba na kuelekea msituni. Alipofika huko, alivutiwa na mazingira ya porini. Kulikuwa na vyakula vingi. Aliona mtama, ndizi na hata ngano. Moyoni aliwaza kwamba chakula hicho kingemfaa yeye na Binadamu. Aliujaza mkoba wake chakula na kurejea nyumbani. Binadamu alifurahi na kushukuru. Baada ya kula, walishauriana. Walikubaliana kwamba Kanga aishi msituni. Tangu siku hiyo, Kanga anaishi msituni. Kila mara alimtembelea Binadamu huku amembebea chakula.

5. Binadamu alimpa Kanga:

______________________________________________________________

6. Kanga ni rafiki wa kweli kwa sababu

______________________________________________________________

7. Kiangazi kilisababisha kukauka kwa ardhi na kukosekana kwa maji na chakula. Je, unadhani kiangazi kilileta hasara gani nyingine kwa binadamu?

______________________________________________________________

*8.* Maana ya **kitatufaa** ni______________________________________________

**Swali la 9 hadi la 12**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Kuna mavazi ya aina nyingi. Mavazi haya huvaliwa kutegemea mahali, wakati na shughuli maalum. Kwa mfano, kuna mavazi ya shuleni. Haya huitwa sare. Kuna mavazi ya kazini na yale tunayovaa tukiwa nyumbani.

Unapochagua mavazi utakayovaa, utazingatia mambo tofauti tofauti. Wakati wa baridi **tunahitaji** kuvaa mavazi mazito. Wakati wa joto kali nao tunavaa mavazi mepesi. Sherehe nazo zina mavazi maalum. Bila shaka umewahi kuhudhuria harusi. Je, Bwana na Bibi harusi walikuwa wamevaa mavazi ya aina gani? Je, wewe ulivaa mavazi ya aina gani? Pengine utasema kwamba ulivaa rinda au shati jeupe.

Ni muhimu kuyatunza mavazi yetu. Tuyafue kila mara na kuyaweka mahali safi. Ni vizuri kuyapiga mavazi pasi. Ikiwa huna pasi, yakunje vizuri. Yakiraruka tuyashone. La muhimu zaidi ni kuhakikisha kuwa tunavaa mavazi yenye heshima.

9. Kulingana na aya ya kwanza, mavazi huvaliwa kutegemea

______________________________________________________________

10. Tunaweza kufanya nini ili mavazi yetu yawe ya heshima?

______________________________________________________________

11. Kwa nini watu huvaa mavazi maalum katika sherehe?

______________________________________________________________

 *©2024 The Kenya National Examinations Council*

12. Maana ya **tunahitaji** ni

______________________________________________

**Swali la 13 hadi la 16**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***.**

Jioni moja Yohana na familia yake walikuwa wameketi sebuleni. Walikuwa wanakula chakula cha jioni. Mara walisikia sauti mlangoni.

“Hodi! Hodi!” Mzee Busara alibisha.

Yohana alienda kufungua mlango.

“Karibu, karibu jirani.” Yohana alisema kisha akampisha Mzee Busara ndani. Waliketi kwenye kochi.

“Habari za utokako? Yohana alimuuliza Mzee Busara.

“Njema. Lakini binti yangu ni mgonjwa. Ana homa kali. Imekuja ghafla. Tumempa huduma ya kwanza ila naona anahitaji matibabu zaidi. Naomba unisaidie kumpeleka hospitalini.” Mzee Busara alisema.

Yohana alimpa pole Mzee Busara. Alichukua funguo za gari lake. Aliiaga familia yake na kuondoka na jirani yake. Walipofika nyumbani kwa Mzee Busara, hawakukawia. Walimchukua mtoto na kufululiza hadi hospitalini.

13. Ni nani alibisha mlangoni kwa Yohana?

______________________________________________

14. Yohana ni jirani mwema kwa sababu

______________________________________________

15. Unadhani Yohana alitumia neno gani kuiaga familia yake.

______________________________________________

16. Je, ungekuwa Mzee Busara ungefanya nini baada ya kusaidiwa?


______________________________________________

 *©2024 The Kenya National Examinations Council*

**ZOEZI 4**

**MATUMIZI YA LUGHA**

17. Vikapu hivi vina nomino. Chagua kikapu ambacho kina nomino za ngeli ya U-I pekee.





18. Jaza nafasi kwa kutumia wakati sahihi.

    Maria alipangusa meza jana. Maria a______pangusa meza kesho.

19. Yafuatayo ni maamkuzi. Ni yapi yasiyoambatanishwa ipasavyo?


| | **Maamkuzi** | **Majibu** |
|---|---|---|
| A. | sabalkheri | Aheri |
| B. | Hujambo | njema |
| C. | shikamoo | marahaba |

20. Tazama picha kisha ujibu swali.





Kalamu iko juu ya meza. Mswaki uko __________________________kikombe.





21. Chebet anapanga vitabu kwenye rafu.  Juma ana _____________ sebuleni.

22. Soma sentensi zifuatazo kisha ujibu swali. Fuata mfano.

Mtoto huyu ni mtiifu sana.

**Watoto hawa ni watiifu sana.**

Kikombe chake kina maziwa.

__________________________________________________________


*©2024 The Kenya National Examinations Council*

23. Mwanaisha ameleta kitabu kipya. Jaza pengo kwa jibu sahihi.

    Kitabu kipya_______na mwanaisha ( kimeleta, kimeletwa)

24. Jaza nafasi kwa neno linalofaa.

    Dana ana afya ________ anapata lishe bora.

25. Soma sentensi hizi kisha ujaze pengo. Fuata mfano.

    Maria na Bela wanaruka kamba. Wao wanaruka kamba.

    Kena ametuchorea picha nzuri. ______ametuchorea picha nzuri.

26. Chagua neno sahihi kujaza pengo.

    Mlezi wangu ameninunulia hanchifu___________

    (mpya, jipya )

27. Mwalimu aliwapa wanafunzi kadi za maneno. Je, ni mwanafunzi yupi aliyepewa kadi yenye **vihisishi pekee**?

| **Komu** | **Lisa** | **Matano** |
|---|---|---|
| Imba | kumbe | tena |
| Ruka | Ala! | Hakika |
| Lo! | Lo! | Salaale! |

28. Kamilisha sentensi kwa neno linalofaa. Wanafunzi wanachezea_____________

    (polepole, uwanjani)

29. Rafiki yangu alinitumia barua kupitia kwenye mtandao.

    Neno lingine lenye maana sawa na rafiki ni_____________________________

30. Jirani yenu anakwambia kuwa una bidii kama mlezi wako. Chagua methali ambayo utatumia kumwonyesha kwamba unafuata mfano wa mlezi wako.

    A. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

    B. Mtoto atumwaye ndiye mzuri

 ©2024 The Kenya National Examinations Council

**ZOEZI 5: KUANDIKA**

31. Andika insha kuhusu:

**SHULE YETU**

 *©2024 The Kenya National Examinations Council*

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**


*©2024 The Kenya National Examinations Council*